

Tarehe 3 Machi, 2020

Wapendwa Familia:

Huu umekuwa ni msimu mgumu wa mafua kwa wilaya za shule na jamii kwenye eneo lote la Capital Region. Ninawaandikia kuwaarifu kuhusu hatua ambazo tunaendelea kuchukua kwenye Wilaya ya Shule ya Mji wa Albany ili kutoa mazingira yenye afya kwa wanafunzi na walimu wote, na pia kuwahakikishia kuwa tunafuatilia kile kinachoendelea kuhusu COVID-19, maarufu kama virusi vya corona.

Kama tunavyofanya kwa masuala yanayohusiana na afya, tunafuata mwongozo kutoka kwa Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa vya Marekani, idara za afya za Jimbo la New York na Kaunti ya Albany, na Idara ya Elimu ya Jimbo la New York. Hatuna visa vyovyote vya COVID-19 vilivyoriptiwa kwenye wilaya yetu ya shule, na kufikia tarehe 2 Machi, ripoti zilionyesha kuwa kulikuwa na kisa kimoja cha COVID-19 kilichothibitishwa humu New York.

Hatua ambazo tumechukua katika msimu huu wote wa mafua ni pamoja na kusafisha ili kuua viini kwenye sehemu zinazoshikwa kama vile vishikio vya mlango, viegemeo, kompyuta, mifereji ya maji na sehemu zingine. Tunaendelea kufuata taratibu hizi, na tunakuhimiza kufanya vivyo hivyo nyumbani.

Tungependa pia kushiriki taarifa kuhusu hatua ambazo unaweza kuchukua nyumbani ili kupunguza kusambaa kwa magonjwa mbalimbali, ikiwemo mafua na COVID-19, na kuisaidia familia yako kukaa na afya.

- Nawa mikono yako aghalabu kwa sabuni na maji kwa angalau sekunde 20. Ikiwa sabuni na maji hazipatikani, tumia kiowevu cha kuua viini kwenye mikono. Tumewauliza walimu wakuu wa shule zetu kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wana fursa ya kunawa mikono yako kabla ya chakula cha mchana kila siku, na katika wiki chache zijazo tutakuwa tunaweka vifaa vya kutoa kiowevu cha kuua viini kwenye mikono katika maeneo yenye watu wengi katika kila shule.
- Jua ishara na dalili za mafua - homa, kukohoa, kuwashwa na koo, kutokwa na makamasi au kufungana pua, maumivu ya mwili, kuumwa na kichwa na kuhisi uchovu. Baadhi ya watu huenda pia wakahisi kichefuchefu au kutapika.
- Ikiwa wewe au jamaa wako anaonyesha dalili yoyote kati ya hizi, hasa dalili za ugonjwa wa kupumua, zungumza na mtoa huduma wako wa afya.
- Wafunze watoto wako kufunika midomo yao kwa karatasi ya shashi au sehemu ya ndani ya kiwiko au mkono wao - badala ya viganja vyao - wanapokohoa au kupiga chafya.
- Waache watoto wagonjwa wabaki nyumbani wanapokuwa na dalili za mafua, na kwa saa 24 baada ya mafua kuisha bila kutumia dawa ya kupunguza homa.

KAULI YA DIRA

Wilaya ya Shule ya Mji wa Albany itakuwa ni wilaya ya ubora wa juu zaidi yenye mahusiano yanayojali na uzoefu wa masomo yenye ushirikiano yanayotoa fursa sawa kwa wanafunzi wote kufikia uwezo wao.

KAULI YA DHAMIRA

Tutafanya kazi pamoja kwa ushirikiano na jamii yetu anuwai ili kumshirikisha kila mwanafunzi katika mpango thabiti wa elimu ulioundwa ili kutoa ufahamu na ujuzi unaohitajika kwa mafanikio.

- Wafunze watoto wako kutoshiriki vifaa kama vile miswaki, vinywaji, chakula au vyombo vya kuweka chakula.
- Ikiwa mtoto wako ana matatizo ya kudumu ya afya na anaonyesha dalili kama za mafua, wasiliana na mtoa huduma wako wa afya mara moja.


(ukurasa unaofuata)

Tumejumuisha pia rasilimali muhimu za ziada, na unaweza kutembelea [Sehemu yetu ya Huduma za Afya](https://www.albanyschools.org/healthservices) katika [albanyschools.org/healthservices](https://www.albanyschools.org/healthservices).

- Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa vya Marekani – <https://www.cdc.gov/flu/prevent/index.html>
 - Mafua: Mwongozo wa Wazazi – bit.ly/familyfluguide
 - CDC katika Vitendo: Kuandaa Jamii kwa ajili ya Uwezekano wa Kusambaa kwa COVID-19 – <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/php/preparing-communities.html>
- Idara ya Afya ya Jimbo la New York State – <https://www.health.ny.gov/>
- Simu ya Kupata Maelezo kuhusu Virusi vya Corona katika Jimbo la New York – 888-364-3065

Afya na usalama wa watoto wetu wote ni kipaumbele cha juu kwetu. Wafanyakazi wetu wa Huduma za Afya wataendelea kufanya kazi kwa karibu na idara za afya za kaunti na jimbo ili kufuatilia hali za mafua na pia taarifa zinazoibuka kuhusu COVID-19. Tafadhali zungumza na mwalimu mkuu wa shule yako ikiwa una maswali ya ziada.

Wenu mwaminifu,



Kaweeda G. Adams
Msimamizi wa Shule